

JESHI LA ULINZI LA WANANCHI WA TANZANIA

NAFASI ZA KUJIUNGA NA JESHI

1. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linatangaza nafasi za kujiunga na Jeshi kwa Vijana wa Kitanzania wenye elimu ya kuanzia Kidato cha Nne hadi Shahada ya Uzamili ambao wamemaliza Mkataba wa Mafunzo ya Kujitolea JKT na kurudishwa majumbani.

SIFA ZA MWOMBAJI

2. Vijana wa Kitanzania wenye nia ya kuandikishwa Jeshi wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

a. Awe raia wa Tanzania wa kuzaliwa mwenye Kitambulisho cha Taifa.

b. Awe na umri wa miaka **18** hadi **26** kwa wenye elimu ya Kidato cha Nne hadi Kidato cha Sita na umri usiozidi miaka **27** kwa wenye elimu ya Juu.

c. Awe na afya nzuri na akili timamu.

d. Awe Mtanzania mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia ya makosa ya jinai Mahakamani na kufungwa.

e. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (**Original Birth Certificate**), vyeti vya Shule na vyeti vya Taaluma.

f. Awe hajatumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM).

g. Asiwe ameo au kuolewa.

h. Awe amehitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mkataba wa kujitolea miaka miwili (2) na kutunukiwa cheti. Wale vijana wa JKT waliopo Makambini ambao wana sifa tayari, utaratibu wao wa kuwaandikisha unafanyika tofauti na vijana waliopo majumbani ambao tangazo hili linawahusu.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

3. Maombi yote yaandikwe kwa mkono na yawasilishwe Makao Makuu ya Jeshi Dodoma kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe **20 Machi, 2023** yakiwa na viambatisho vifuatavyo:-

a. Nakala ya Kitambulisho cha Taifa au namba ya **NIDA**.

b. Nakala ya cheti cha kuzaliwa, vyeti vya Shule na Chuo.

c. Nakala ya cheti cha JKT.

d. Namba ya simu ya mkononi ya mwombaji.

MAOMBI YATUMWE KWA ANUANI IFUATAVYO

4.a. Mkuu wa Utumishi,

Makao Makuu ya Jeshi,

Sanduku la Posta 194,

DODOMA, Tanzania.

b.Email: **ulinzimagazine@tpdf.mil.tz**